

- 1** Baadhi ya watoto wanaozaliwa na mpasuko wa mdomo - shimo, pengo, au ufa katika mdomo au shimo katika paa la kinywa (ambayo inaweza kuwa wazi kutoka nje).



- 2** Operesheni ni muhimu sana kwa sababu bila hivyo mtoto hawezi kusema vizuri, hatari za maambukizi yanaongezeka, na anakuwa na matatizo ya kula chakula na kunywa maziwa.



- 3** Daktari mpasuaji wa Smile Train anaweza kurekebisha kasoro hii kwa bure katika hospitali zinazoshirikiana na Smile Train. Upasuaji ni njia pekee ya kikamilifu inayorekebisha kasoro hii.

- 4** Ili kuwa na afya na nguvu ya kutosha operesheni ni muhimu ili watoto wenye mpasuko walishwe vizuri.



- 5** LAKINI - wakati mwingine ni vigumu kuwalisha watoto wenye mpasuko wa mdomo kwa sababu maziwa yanaweza kutoka puani au yanaweza kuingia kwenye mapafu yao. Au pia watoto wanaweza kuvuta hewa nyingi, na wanaweza kuonekana wameshiba na kulala usingizi hata kama hawajashiba vizuri.




- 6** Ni muhimu mtoto ashibe vizuri ili aweze kufanyia operesheni. Wakina mama wanatakiwa kujaribu njia mbali mbali za kumlisha mtoto. Ni vizuri kumyonyesha mtoto moja kwa moja kutoka maziwa ya kifua, kama inawezekana. Zifuatazo ni njia tofauti:



Nyonyesha mtoto akiwa amekeaa wima wima.



Mpe chuchu upande wa mdomo usio na mpasuko.



Minya taratibu matiti kuongeza mzunguko wa maziwa.



Lisha mtoto na hakikisha anacheua mara nyingi sana.

- 7** Kama haiwezekani kumyonyesha maziwa ya kifua, ni jambo la muhimu mama aendelee kumlisha mtoto kwa kutumia njia nyingine. Baadhi ya njia hizi ni:




Mama anaweza kumpa mtoto maziwa ya kifua kwa kutumia kijiko au chupa.



Mama anaweza kupanua KIDOGO shimo la chuchu ya chupa ya maziwa ili kuongeza mzunguko wa maziwa.

- 8** Kama maziwa ya kifua hayatoki, mama anaweza kumyonyesha mtoto maziwa ya ng'ombe au formula. Hakikisha maziwa ya ng'ombe na maji ya formula yamechemshwa na kisha kupozwa.



- 9** Hakikisha vifaa vyote vinavyotumika kumlisha mtoto ni visafi na vimechemshwa katika maji kwa dakika 10. Vijiko vichafu na chupa chafu zinaweza kusababisha homa na maambukizi.



- 10** Tafadhali usisahau kumpeleka mtoto wako kituo cha karibu cha Smile Train. Daktari wa kituo atamchunguza mtoto na kukueleza lini anatakiwa kuja hospitali ili afanyiwe operesheni ya upasuaji.

Kumbuka, matibabu yote yanayofanywa katika kituo chochote cha Smile Train ni bure kabisa.

